



Australian Red Cross
THE POWER OF HUMANITY

Msaada wa Dharura wa COVID-19

Australian Red Cross imefadhiliwa kwa ajili ya kutoa misaada ya dharura kwa watu walio kwenye visa za muda mfupi hapa Australia Magharibi (Western Australia) ambao wameathirika na janga la COVID-19.

Red Cross inawezaje kunisaidia?

Red Cross inatoa mifuko ya chakula na malipo ya mara moja tu kwa mahjitaji ya haraka ya kifedha. Vile vile tunaweza kukusaidia na usimamizi wa kesi yako pamoja na malipo ya kuendelea ikiwa uko katika hali ngumu sana.

Je, nitaweza kuupata msaada huu?

Unaweza kuupata Msaada wa Dharura wa Red Cross kama:

- Wewe sio raia wa Australia au mkazi wa kudumu
- Una mahitaji ya muhimu kama vile chakula, na
- Hauna kipato wala akiba ya kukidhi mahitaji yako.

Je, nawezaje kujiandikisha kuomba msaada huu?

Kupata msaada huu, lazima uombe kupitia tovuti yetu:

www.redcross.org.au/emergencyrelief

Kabla ya kuanza ombi lako utahitaji kuandaa hati za kuambatisha. Hati hizi ni:

- Ushuhuda wa (hali ya) visa yako kwa mfano, nambari ya pasipoti
- Hati ya benki inayoonyesha jina lako kama mwenye akaunti, nambari ya tawi (BSB) na nambari ya akaunti.

Ikiwa hauna uhakika au visa halali hivi sasa, bado unaweza kuomba usaidizi na tutawasiliana nawe kujadili ombi lako.



Australian Red Cross

THE POWER OF HUMANITY

Je, kwanini unatak habari zangu za kibinafsi?

Tutakusaidia kwa kulingana na mahitaji yako, sio hali ya visa yako. Tunakuomba utupe habari zako za kibinafsi ili tukusaidie. Tunatoa habari hizi kwa watu au mashirika mengine, au serikali ukitupa ruhusa, au tukiitishwa kwa sababu za kisheria.

Je, nikihitaji msaada kujaza fomu nifanyeje?

Mtoa huduma yeyote anaweza akakusaidia kuijaza fomu kwenye mtandao. Watu wa Red Cross vile vile wanatoa msaada wa kujaza fomu – tunapatikana:

- Kanisa la Riverview kwenye **Asylum Seeker Hub** (Anuani ni 1 Thorogood Street Burswood) **kati ya saa 8 na saa 11 jioni kila Jumanne**, au
- **Ofisi ya Red Cross** (Anuani ni 110 Goderich Street East Perth) kati ya **saa 3 na saa 5 asubui kila Alhamisi**.

Vile vile unaweza ukatuma barua pepe (email) wamsphub@redcross.org.au ukiomba usaidizi. Hakikisha umeweka namba yako ya simu kisha mmoja wetu atakupigia haraka uwezekanavyo.

Je, nini kinafuata baada ya kuwatumia ombi langu la malipo?

Utapigiwa simu kutoka Red Cross kukuulizwa maswali ya kutathmini aina gani ya msaada unahitaji.

Je, itachukua muda gani kupokea malipo yangu?

Kwa sasa tunapokea maombi mengi ya malipo haya, na tunajitahidi kuyafanyia yote kazi haraka iwezekanavyo. Baada ya kututumia ombi lako, unaweza kutuma barua pepe wamsphub@redcross.org.au kuomba kadiri la tarehe ya malipo kukufikia.



Australian Government
Department of Social Services

